TANGAZO LA SERIKALI NA 780 la tarehe 18/9/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI ZA WILAYA YA HANDENI ZA MWAKA 2020

Jina

**1.** Sheria Ndogo hizi itajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya Handeni za Mwaka 2020.

Tafsiri

**2.** Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale muktadh umeeleza vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Handeni;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, phelispa, quartz,morram, mawe meupe, kokoto, mawe na matofali;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri; na

"wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya

ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

Utozaji wa ada na ushuru

**3.-** (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

**4.** Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

**5.-** (1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria

**6.-** (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo

Ndogo

itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru na atapaswa kujaza fomu maalumu kama inavyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

**7.-** (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa

**8.** Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au

Mwidhiniwa

chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu

**9.-** (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha kwanza atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufililisha kosa

**10.-** Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 3(1))*

**SEHEMU YA KWANZA**

Ada ya Kukodisha Mali za Halmashauri

| **Na.** | **Aina ya chanzo** | **Kiasi cha ushuru** |
|---|---|---|
| 1 | Kumbi za Halmashauri<br>(a) ukumbi mkubwa<br>(b) ukumbi mdogo | <br>Tshs. 200,000 kwa siku<br>Tshs. 100,000 kwa siku |
| 2 | Mitambo | Tshs. 50,000 kwa saa |
| 3 | Nyumba- biashara | Kulingana na Mkataba |
| 4 | Nyumba ya kuishi (ambayo siyo ya watumishi) | Kulingana na mkataba |
| 5 | Uwanja wa mikutano | Tshs. 100,000 kwa siku |
| 6 | Vizimba | Tshs. 2000 kwa mita 1 ya Mmraba |
| 7 | Viti vya Halmashauri-<br>(a) vya plastiki<br>(b) vya mbao<br>(c) vya kwisheni | <br>Tshs. 500 kwa kiti kwa siku<br>Tshs. 300 kwa kiti kwa siku<br>Tshs. 1,000 kwa kiti kwa siku |

**SEHEMU YA PILI**

ADA YA VIBALI MBALIMBALI

**I**

| **Na.** | **Aina ya Kibali** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kuweka uzio/fensi ya muda kwa ajili ya kufanya ujenzi ili kulinda usalama wa watu na mali. | -Ujazo mdogo ( low density) - 120,000/=<br>-Ujazo wa kati ( medium density) - 75,000/=<br>-Ujazo mkubwa ( high density) - 30,000/= |
| 2. | Kibali cha kufanya matangazo ya biashara maeneo mengine nje na minada, masoko na magulio. | Shilingi 50,000/= Kwa siku |
| 3. | Ada ya usimikaji bango la biashara katika barabara za Halmashauri. | Shilingi 30,000/= kwa kila bango |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Kibali cha mazishi (maeneo ya kuzikia yanayomilikiwa na Serikali) | 10,000/= |
| 5. | Kibali kwa ajili ya shughuli za kiutamaduni | (a) matangazo na burudani mbalimbali- Tsh 10,000/= kwa siku ndani ya Kata<br>(a) Matangazo na burudani mbalimbali –Tsh 40,000/= kwa siku ndani Halmashauri.<br>(b) Kupiga mziki katika baa na kumbi ni Tsh.10,000 kwa siku<br>(c) Ushuru wa huduma kwa mashine za bahati nasibu ni asilimia 0.03 ya mapato kwa siku<br>(d) Ada ya usajili waganga wa jadi/tiba mbadala – Tsh 50,000/= kwa mwaka. |
| 8 | Ada ya usajili wa vikundi vya kijamii (CBOs) | Tsh 30,000/= |
| 9 | Vikundi vingine ambavyo havijatajwa | Tsh 10,000/= |
| 10 | Ada ya usajili wa fundi atakayekuwa akifanya kazi za ujenzi Halmashauri | 50,000/= |

## SEHEMU YA TATU

Ushuru wa mifugo minadani

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Tsh.4,000/= |
| 2. | Mbuzi | Tsh. 1,000/= |
| 3. | Kondoo | Tsh.1,000/= |
| 4. | Nguruwe | Tsh.1000/= |
| 5. | Punda. | Tsh.4,000/= |
| 6. | Kuku | Tsh.500/= |
| 7. | Ngozi ya ng'ombe | Tsh.500/= |
| 8. | Ngozi ya mbuzi | Tsh.200/= |
| 9. | Ngozi ya kondoo | Tsh.200/= |

## SEHEMU YA NNE

Ada ya Ununuzi wa Vitabu vya Zabuni

| NA | AINA YA VITABU | KIWANGO CHA ADA |
|---|---|---|
| **1** | Kitabu cha Zabuni | Tshs. 100,000 endapo thamani ya Zabuni ni chini ya Bilioni 1 |
| **2** | Kitabu cha Zabuni | Tshs. 150, 000 endapo thamani ya Zabuni ni zaidi ya Bilioni 1 |

## SEHEMU YA TANO

### A: VIBALI VYA UJENZI

| MITA ZA ENEO | MITA ZA ENEO | JUMLA YA ENEO LINALZIDI | JUMLA YA ENEO LISILOZIDI | VIWANJA VIKUBWA(LOW DENSITY) | VIWANJA UKUBWA WAKATI(MEDIUM DENSITY) | VIWANJA VIDOGO(HIGH DENCITY AREA) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KIASI TSHS | KIASI TSHS | KIASI TSHS |
| | 500 $m^2$ | | 49.45$m^2$ | 7,500.00 | 4,500.00 | 1,500.00 |
| 500 $m^2$ | 1000 $m^2$ | 46.45 $m^2$ | 92.9 $m^2$ | 12,000.00 | 7,000.00 | 3,000.00 |
| 1000 $m^2$ | 1500 $m^2$ | 92.9 $m^2$ | 139.35 $m^2$ | 15,000.00 | 9,000.00 | 5,000.00 |
| 1500 $m^2$ | 2000 $m^2$ | 139.35 $m^2$ | 185.8 $m^2$ | 23,000.00 | 12,000.00 | 7,000.00 |
| 2000 $m^2$ | 3000 $m^2$ | 185.8 $m^2$ | 278.7 $m^2$ | 30,000.00 | 23,000.00 | 8,000.00 |
| 3000 $m^2$ | 4000 $m^2$ | 278.7 $m^2$ | 371.6 $m^2$ | 45,000.00 | 30,000.00 | 18,000.00 |
| 4000 $m^2$ | 5000 $m^2$ | 371.6 $m^2$ | 464.5 $m^2$ | 60,000.00 | 38,000.00 | 30,000.00 |
| 5000 $m^2$ | 6000 $m^2$ | 464.5 $m^2$ | 557.4 $m^2$ | 75,000.00 | 52,000.00 | 38,000.00 |
| 6000 $m^2$ | 7000 $m^2$ | 557.4 $m^2$ | 650.3 $m^2$ | 90,000.00 | 62,000.00 | 45,000.00 |
| 7000 $m^2$ | 10000 $m^2$ | 650$m^2$ | 929 $m^2$ | 200,000.00 | 120,000.00 | 53,000.00 |
| | | KIASI KINACHOONGEZEKA KWA KILA 92.902SQM ZINAZOZIDI | | 8,500.00 | 7,500.00 | 2,000.00 |

### B: KIBALI CHA KUJENGA UZIO WA KUDUMU

| Na. | Ukubwa wa eneo | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | 100$m^2$ hadi 600$m^2$ | 45,000/= |
| 2. | 601$m^2$ hadi 1600$m^2$ | 75,000/= |
| 3. | 1601$m^2$ hadi 4000$m^2$ | 150,000/= |
| 4. | 4001$m^2$ hadi 6000$m^2$ | 300,000/= |
| 5. | Zaidi ya 6001$m^2$ | 450,000/= |

### C: KIBALI CHA KUJENGA MINARA YA MAWASILIANO KWENYE MAENEO YA HALMASHAURI (INSTALLATION CHARGES)

| Na. | Idadi | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | Kila mnara mmoja | 2,000,000/= |

D: KIBALI CHA UKARABATI WA MAJENGO

| | |
|---|---|
| Ada ya kibali cha ukarabati | 500,000/= |

**SEHEMU YA SITA**
**Ada ya minara ya mawasiliano**

1. Mnara uliojengwa kwenye eneo linalomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya Tsh. 5,000,000/= kwa mwezi.
2. Mnara uliojengwa kwenye eneo linalomilikiwa na Halmashauri ya Kijiji Tsh. 3,000,000/= kwa mwezi.

**SEHEMU YA SABA**

Upandikizaji wa mbegu kwa mifugo na uogeshaji wa mifugo

| **NA** | **AINA YA MFUGO** | **KIWANGO CHA ADA** |
|---|---|---|
| 1 | Upandikizaji wa Ng’ombe | Tshs. 20,000 kwa ng’ombe |
| 2 | Uogeshaji wa- | |
| | (a) Ng’ombe | Tshs. 200 mmoja |
| | (b) Mbuzi | Tshs. 100 mmoja |
| | (c) Kondoo | Tshs. 100 mmoja |
| | (d) Punda | Tshs. 200 mmoja |

**SEHEMU YA NANE**
**Ushuru wa Madini ya Ujenzi**

| Na, | AINA YA MADINI | KIWANGO CHA USHURU. |
|---|---|---|
| 1. | Kokoto za kujengea za aina zote | Tsh.1,500/= kwa tani |
| 2. | Mawe ya phelispa na quartz | Tsh.1,000/= kwa tani. |
| 3. | Mchanga wa kujengea | Tsh.1,000/= kwa tani. |
| 4. | Vumbi la kokoto na morram | Tsh.1,000/= kwa tani |
| 5. | Mawe meupe (dolomite) | Tsh.1,000/= kwa tani |
| 6. | Mawe ya kujengea aina | Tsh.1,000/= kwa tani |

| | | |
|---|---|---|
| | zote | |
| 7. | Kifusi | Tsh.1,000/= kwa tani |
| 8. | Madini ya chuma | Tsh 1,000/= |

**SEHEMU YA TISA**
**Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa Nyama**

| Na | AINA YA MFUGO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Ukaguzi wa nyama<br>(i) ng'ombe<br>(ii) mbuzi<br>(iii) kondoo<br>(iv) nguruwe<br>(v) kuku<br>(vi) bata | <br>Tshs. 5,000/=<br>Tshs. 5,000/=<br>Tshs. 5,000/=<br>Tshs. 5,000/=<br>Tshs. 10,000/=<br>Tshs.5,000/= |

**SEHEMU YA KUMI**

**Ushuru wa mazao**

1. **Mazao ya biashara** **Asilimia 3 ya bei ya soko.**
2. **Mazao ya chakula** **Asilimia 3 ya bei ya soko.**

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**
**Ushuru wa Mazao ya Misitu**

| Na | AINA YA MAZAO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Uuzaji wa Mbao katika chanzo | Asilimiia 5 ya ujazo |
| 2 | Uuzaji wa Mkaa katika chanzo | Asilimiia 5 ya ujazo |
| 3 | Uuzaji wa Magogo katika chanzo | Asilimiia 5 ya ujazo |
| 4 | Uuzaji wa Mirunda katika chanzo | Asilimiia 5 ya ujazo |
| 5 | Uuzaji wa kuni katika chanzo | Asilimiia 5 ya ujazo |
| | Uuzaji wa fito | Asilimiia 5 ya ujazo |

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**
Uuzaji wa Mbegu zinazozalishwa na Halamshauri

| Na | UJAZO WA MBEGU | KIWANGO CHA FEDHA |
|---|---|---|
| 1 | Mahindi | Tshs. 2000 kwa kilo moja |
| 2 | Mhogo | Tshs. 100 kwa mche mmoja |
| 3 | Korosho | Tshs. 200 kwa mche mmoja |
| 4 | Ufuta | Tshs. 3000 kwa kilo moja |
| 5 | Mtama | Tshs. 500 kwa kilo moja |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Na mbegu nyingine ambazo hazijatajwa | Tshs. 2000 kwa kilo |

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

### Tozo kwa mifugo inayozurura ovyo

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | Tsh.2,000/= kwa siku |
| 2. | Mbuzi | Tsh.2,000/= kwa siku |
| 3. | Kondooo | Tsh.2,000/=kwa siku |
| 4. | Punda | Tsh.2,000/=kwa siku |
| 5. | Mbwa | Tsh.5,000/=kwa siku |
| 6. | Nguruwe | Tsh.2,000/= kwa siku |

## SEHEMU YA KUMI NA NNE

ADA ZA UKUSANYAJI TAKA KATIKA KAYA,TAASISI NA MAJENGO YA BIASHARA

| | AINA YA BIASHARA/JENGO | | VIWANGO VYA ADA | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| | Makazi (kaya) | | 2,000/= | Kwa mwezi |
| | Mgahawa | Mdogo | 2,000/= | Kwa mwezi |
| | | wa kati | 3,000/= | Kwa mwezi |
| | | Mkubwa | 3,000/= | Kwa mwezi |
| | Nyumba za kulala wageni | za kawaida | 2,000/= | Kwa mwezi |
| | | za kitalii | 3,000/= | Kwa mwezi |
| | Mduka ya kufulia nguo(dry cleaner) | | 2,000/= | Kwa mwezi |
| | Grocery | | 3,000/= | Kwa mwezi |
| | Baa | | 3,000/= | Kwa mwezi |
| | Duka la jumla | | 5,000/= | Kwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | mwezi |
| | Duka la rejareja | 3000/= | Kwa mwezi |
| | Shule ya msingi ya bweni | 5,000/= | Kwa mwezi |
| | Shule ya sekondari ya bweni | 5,000/= | Kwa mwezi |
| | Klabu ya usiku | 2,000/ | Kwa mwezi |
| | Kumbi za sherehe | 4,000/ | Kwa mwezi |
| | Zahanati (taka zisizohatarishi) | 5,000/= | Kwa mwezi |
| | Kituo cha afya (taka zisizohatarishi) | 10,000/= | Kwa mwezi |
| | Hospitali (taka zisizohatarishi) | 20,000/= | Kwa mwezi |
| | Nyumba za sinema | 3,000/= | Kwa mwezi |
| | Stoo za mkaa | 4000/= | Kwa mwezi |
| | Kituo cha michezo | 3000/= | Kwa mwezi |
| | Klabu ya pombe za asili | 2000/= | Kwa mwezi |
| | Taasisi mbalimbali | 5000/= | Kwa mwezi |
| | Ghala | 3,000/= | Kwa mwezi |
| | Stoo | 2000/= | Kwa mwezi |
| | Kituo cha kuuza mafuta | 5000/= | Kwa mwezi |
| | Saluni | 3000/= | Kwa mwezi |
| | Fundi wa vifaa vya umeme | 3000/= | Kwa mwezi |
| | Duka la kuuza nyama na samaki | 3000/= | Kwa mwezi |
| | Depo | 5000/= | Kwa mwezi |
| | Maduka ya vifaa vya ofisi (stationary) | 2000/= | Kwa mwezi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Wauza mkaa jumla | | 4,000/= | Kwa mwezi |
| | Vibanda vya simu | | 1000/= | Kwa mwezi |
| | Mashine za kusaga na kukoboa | | 1000/= | Kwa mwezi |
| | Mashine za kusaga na kufunga unga | | 3000/= | Kwa mwezi |
| | Sehemu za kuosha magari | ndogo | 2000/= | Kwa mwezi |
| | | kubwa | 4000/= | Kwa mwezi |
| | Gereji za magari | | 2000/= | Kwa mwezi |
| | Gereji za pikipiki | | 1000/= | Kwa mwezi |
| | Viwanda | vidogo | 5,000/= | Kwa mwezi |
| | | vikubwa | 10,000/= | Kwa mwezi |
| | Karakana | | 5,000/= | Kwa mwezi |

GHARAMA ZA UBOMOAJI NA UONDOAJI WA MABAKI YA VIFAA VYA UJENZI

| Na. | Eneo kwa mita ya ujazo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mita moja ya mraba | 5,000/= |
| | | |

GHARAMA ZA UTUPAJI TAKA NGUMU KWENYE JAA LA TAKA

| Na. | Kiasi cha taka | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Chini ya tani moja kwa safari | 40,000/= |
| 2 | Zaidi ya tani moja kwa safari | 50,000/= |

GHARAMA ZA UTUPAJI MAJI TAKA KWENYE BWAWA LA MAJI TAKA

| Na. | Kiasi cha maji taka | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Chini ya tani moja kwa safari | 40,000/= |
| 2 | Zaidi ya tani moja kwa safari | 50,000/= |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 6 (2))*

**FOMU YA KUKAMATA MALI**

**HATI NA. ………….** **Tarehe…….……………….**

Mimi…………………………………… ambaye ni afisa mwidhiniwa nathibitisha kukamata mali Zifuatazo: -
1.…………………………….
2…………………………….
3……………………………
4…………………………….
Ambazo zinamilikiwa na bwana/bibi……………..………. leo hii tarehe………... saa……………. hapa…………. (mahali) kwa kosa la …………………………….

Saini……………….

Mmiliki wa mali
Jina………………………………………..……..
Sahihi……………………………………………
Tarehe………………………….

NB; Fomu hii ijazwe nakala mbili: - nakala moja kwa ajili ya afisa mwidhiniwa na nakala ya pili kwa mmiliki wa mali.

## JEDWALI LA TATU

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 10)*

**KUFILILISHA KOSA**

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Handeni za mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya ya Handeni, Niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………………. ya mwezi…………………. mwaka…………………

Jina…………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina……………………………………...cheo…………………………………….

Saini……………………………………tarehe……………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya Handeni imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliyofanyika mnamo tarehe 20………mwezi ……….2020 mbele ya:

......................................
WILLIAM M. MAKUFWE.
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Handeni

..…………………
MUSTAFA S. BELEKO.
Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Handeni

**NAKUBALI**

………………………………
SULEIMANI JAFFO
WAZIRI WA NCHI-OR-TAMISEMI

DODOMA

Tarehe 01 Septemba, 2020